


Rainwater harvesting system

Mfumo wa uvunaji maji ya mvua



Cleaning the gutter
Kusafisha kingamaji

Kitini elekezi cha jinsi ya kusafisha tenki la kuvunia na kuhifadhi maji ya mvua

Ukarabati wa tenki la kuvunia maji ya mvua

Tenki la kuvunia na kuhifadhi maji ya mvua linaweza kutupatia maji safi na salama endapo yafuatayo yatazongatiwa:

Kabla mvua haijanyesha:

Safisha tenki

Safisha paa la nyumba

Safisha kinga maji zote

Safisha chujio

Safisha bomba linaloelekea chini

Kipindi cha mvua kikianza:

Mvua za mwanzo kabisa zitaondoa uchafu wowote uliokuwepo kwenye paa na katika kinga maji za nyumba. Uchafu huo utatokea kwenye bomba linaloelekea chini. Pindi bomba linaloelekea chini litakapojaa, maji yataanza kuingia kwenye tenki.

Kipindi mvua zinapokuwa zinaendelea kunyesha

Maji yanayokuwepo kwenye bomba linaloelekea chini yatatoka taratibu kupitia tundu dogo lililopo kwenye ncha ya bomba hilo. Hili linafanyika kuhakikisha kuwa, uchafu hautarudi/ hauingii kwenye tenki.

Mambo ya kufanya mara kwa mara kipindi mvua zinaendelea kunyesha

- Fungua bomba liendalo chini baada ya mvua
- Kagua na safisha paa la nyumba
- Kagua na safisha kinga maji
- Kagua na safisha chujio
- Kagua na safisha bomba liendalo chini

Kipindi cha mvua za mwisho (Tenki limejaa)

Maandalizi yafanyike kuhakikisha kuwa maji safi na salama ya kunywa yanakuwepo kwa nagalau mwezi mmoja unaofuata

Jambo la kufanya wakati msimu wa mvua umeisha (wakati tenki limejaa)

- Hakikisha mfuniko umefungwa vizuri
- Hakikisha hakuna wanyama, wadudu au mwanga haupenyi ndani ya tenki kwani hili litaharibu ubora wa maji.

